


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**  
**SHULE YA SEKONDARI DENDEGO**



SIMU: 0789160787,  
 0622333041,  
 0675468465.

EMAIL:- [sdendego@gmail.com](mailto:sdendego@gmail.com)

Ofisi ya Mkuu wa Shule,  
 S.L.P 23,  
 Kilosa.  
**14 DESEMBA, 2020**

**KUMB:NO.KDC/DSS/2020/VOL.01.**

JINA LA MWANAFUNZI .....  
 S. L. P. 170,  
**KILOSA.**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI**  
**DENDEGO KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

**1.0 UTANGULIZI.**

- ✓ Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga **Kidato cha Kwanza** katika Shule hii **Mwaka 2020**. Shule hii ipo eneo la **Mlimani Boma Kata ya Kasiki Tarafa ya Kilosa Mjini** karibu na **Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa**, Umbali ni Kilometa moja (01Km) na nusu (500M) kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.
- ✓ Muhula wa kuanza masomo unaanza **tarehe 11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia **Tarehe 6/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni **tarehe 15/01/2021**. (Ndani ya siku saba za kazi) "**KUTORIPOTI SHULENI NI KOSA KISHERIA, HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA KWA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI ATAKAYEKIUKA.**"

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 SARE ZA SHULE**

(a) Sare ya shule hii ni:-

- i) **Wavulana**; Suruali mbili (02) pana na Shati mbili (02) nyeupe za tetron mikono mifupi aina ya tomato, soksi nyeusi na viatu vya ngozi vyeusi vya vya kufunga na kamba. **(ISIWE RABA)**
- ii) **Wasichana**; Sketi mbili (02) ndefu ya kufika kwenye kifundo cha Mguu na Shati mbili (02) nyeupe za tetron mikono mifupi aina ya tomato, soksi nyeupe na viatu vya ngozi vyeusi vya vya kufunga na kamba. **(ISIWE RABA)** Mshono wa Sketi ni linda box.

**FORM ONE JOINING INSTRUCTION FOR ACCADEMIC YEAR 2021**

**NB: "Kitambaa cha rangi ya sketi na suruali kimeambatanishwa. Rangi ya hijab kwa wasichana ifanane na sare ya shule."**

(b) Sare za Michezo ni:-

- i) **Wavulana** ;Tisheti ya Zambarau, Kaptura au Bukta ya Zambarau na Track suit za Zambarau.
- ii) **Wasichana** ; Tisheti ya Zambarau , Kaptura au Bukta ya Zambarau na Track suit za Zambarau.

## **2.2 VIFAA VYA DARASANI**

- ✓ Daftari aina ya Counter Book kumi(10), Daftari kubwa za kawaida (msomi) kumi (10) kwaajili ya mazoezi, Kalamu za wino za kutosha, Mkebe wa Hesabu(Mathematical Set), Penseli, Graph Pads na Rula.

## **2.3 VITABU VYA TAFSIRI YA LUGHA(DICTIONARY) MBILI,**

- ✓ Moja ya Kiingereza- Kiswahili na ya pili ni ya Kiswahili – Kiingereza. (English – Swahili Dictionary na Swahili – English Dictionary)

✓

## **2.4 Chakula cha mchana, matibabu ya na vifaa vya usafi kwa wasichana ni gharama ya mzazi.**

## **2.5 Mahitaji Mengine ni pamoja na Jembe au kwanja na Fagio.**

### **NB; "MUHIMU SANA"**

- ✓ Mwanafunzi anapokuja kuripoti shuleni ni lazima awe amevaa sare ya shule iliyokamilika(fuul uniform) pia aje na vifaa na mahitaji yote ya shule kama ilivyoelekezwa.
- ✓ Mwanafunzi atakayekuja kuripoti shuleni akiwa kavaa nguo za nyumbani au hana mahitaji yaliyoelekezwa hatosajiliwa/ hatopokelewa.

## **3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.**

- ✓ Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa **Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978** na kama ilivyorekebishwa kwa **Sheria namba 10 ya mwaka 1995**. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na **Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Elimu ya juu** yenye dhamana ya Elimu chini ya **Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu nchini.
- ✓ Unatakiwa kuzingatia **Sheria, Taratibu, Kanuni** na mambo mengine ya msingi utakayoelekezwa ukiwa shuleni.
- ✓ Zifuatazo ndio sheria za shule:-

### **3.1 Sheria za jumla**

- ✓ Uvunjaji wa sheria zifuatazo utapelekea mwanafunzi kupewa adhabu kali na marudio yake yatasababisha mwanafunzi kusimamishwa masomo:-

**FORM ONE JOINING INSTRUCTION FOR ACCADEMIC YEAR 2021**

- i.** Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi/walezi, wafanyakazi wasio walimu na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima. Ni lazima mwanafunzi asimame anapopita mwalimu, mzazi n.k na asalimie na kisha apokee vifaa alivyonavyo. Vilevile wanafunzi wanatakiwa kuheshimiana na kushirikiana.
- ii.** Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- iii.** Kushiriki kwa umakini katika kufanya maandalio ya jioni.(Preparation). Ni lazima kali mwanafunzi awe na ratiba ya kujisomea nyumbani.
- iv.** Kuwahi katika shughuli za shule na kazi nyingine utakazopewa ni jambo la lazima.
- v.** Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii. Ukitoka nje ya mipaka ya shule ni lazima uwe na kibali.
- vi.** Kutunza usafi wa mwili, malazi na mazingira ya shule ni lazima kwa kila mwanafunzi. Hii ni pamoja na kuokota uchafu ulio karibu yake.
- vii.** Kuvaa sare ya shule wakati wote na ni lazima shati/tshirt ichomekwe kwenye sketi/suruali . ni mamarufuku kuvaa viatu vya wazi (ndala/malapa/sendu) shuleni.
- viii.** Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- ix.** Kutunza mali za umma, za shule, zake binafsi na wazenzake. Mwanafunzi atalazimika kufidia mali yoyote atakayo haribu au kupoteza.
- x.** Wanafunzi ni lazima waheshimu Ofisi ya Mkuu wa Shule, ofisi za idara, ofisi ya mwalimu, ukumbi wa chakula, maabara, maktaba na madarasa.
- xi.** Kuhudhuria masomo kwa wakati, kuandika nukuu za masomo, kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote inayomuhusu, na kama kuna sababu ya kutohudhuria darasani au kufanya zoezi jaribio au mtihani ielezwe mapema.
- xii.** Kutii kengele kama mwito wa haraka. Mwanafunzi ni lazima akimbie kuelekea eneo la mkusanyiko au eneo husika mara tu asikiapo kengele.

### **3.2 Sheria za Madarasani**

- ✓ Ukiukaji wa sheria hizi utasabisha mwanafunzi kupewa adhabu kali:-
  - i.** kelele za aina yoyote haziruhusiwi darasani. Kumbuka darasani ni mahali pa kujifunzia, sio pa kupiga kelele.
  - ii.** Ni lazima kila mwanafunzi akae darasani kwa kufuata mpango uliowekwa, kutofanya hivyo ni kukiuka sheria.
  - iii.** Hakuna mwanafunzi atakayetoka nje ya darasa wakati wa vipindi bila ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa.
  - iv.** Ni marufuku kuingia na chakula/kinywaji darasani au kula darasani.
  - v.** Ni marufuku mwanafunzi yeyote kuandika maandishi yoyote kwenye dawati, kiti, meza, sakafu, kuta au paa za darasa/ofisi. Adhabu kali itatolewa kwa atakaebainika kufanya hivyo.

### 3.3 Makosa yafuatayo yatasababisha mwanafunzi afukuzwe shule

- i. Wizi wa aina yoyote ile, hata wa kalamu au daftari.
- ii. Uasherati, ubakaji, usagaji na ushoga.
- iii. Uvutaji wa sigara, bangi, ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyu.
- iv. Kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mtu yeyote iwe shuleni au nyumbani.
- v. Kuoa au kuolewa. Kupata mimba, kusababisha mimba, kutoa mimba, au kusaidia utoaji wa mimba.
- vi. Makosa ya jinai. Mfano kumtishia mwenzako kwa kumwambia "utaona!"
- vii. Kudhihaki/kukejeli/kukashifu imani ya dini/imani yoyote au kuanzisha mabishano na midahalo inayogusa imani za watu wengine.
- viii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- ix. Kughushi nyaraka za shule kama mihuri, saine ya mwalimu, nembo ya shule n.k
- x. Kudharau Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa au Fedha ya Taifa.
- xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama shuleni.
- xii. Kukataa adhabu kwa makusudi bila kujali nani ametoa adhabu hiyo, mwalimu au kiranja.
- xiii. Kupigana na mwanafunzi mwezako, mwalimu na mtumishi asiyekuwa mwalimu.
- xiv. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
- xv. Kutoa lugha chafu/kejeli/matusi kwa wanafunzi wenzako, mwalimu, mzazi, /mlezi au mtumishi asiyekuwa mwalimu ndani au nje ya shule.
- xvi. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni (Gest House). Hii ni pamoja na kuuza pombe au bangi mahali popote pale ilimradi umeonekana.
- xvii. Kuwa au Kumiliki simu ya mkononi.

### 3.4 Nimarufuku kufanya yafuatayo:-

- i. kusuka nywele, kufuga nywele ndefu, kufuga ndevu, kunyoa upara au minyoo ya kihuni/isiyokubalika. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi muda wote.
- ii. Kupaka rangi za nywele, kupaka wanja, kupaka rangi za midomo au kubandika meno ya bandia.
- iii. Kufuga kucha ndefu, kupaka rangi kucha au kubandika kucha za bandia.
- iv. Kujichora michoro (tattoo/ maua mwilini)
- v. Kuvaa shanga, mkufu, heleni, bangili, pete, kacha, rozali/tasbihi, kofia, wigi, ama kirembe.
- vi. Kujiremba, kutumia vipodozi vinavyobadilisha rangi ya ngozi au angel face.
- vii. Kuvaa kanga, gauni, dila, sketi au suruali za kubana, / jeans, fulana/blauzi za mabega wazi wakati wa masomo ya ziada/ maandalizi hasa jioni au siku za wikiendi. Wakati wa masomo ya ziada ni lazima mwanafunzi avae suruali/sketi ya shule na T-shirt ya shule.

**NB:- MHIMU SANA,**

5

**“Mwanafunzi anatakiwa kuwa msafi na nadhifu muda wote awapo shuleni, avae sare ya shule inavyo stahili na ni marufuku kuvaa mlegezo.”**

**4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa na mwanafunzi shuleni ni pamoja na;**


- (a) **Medical Examination Form**, ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule utapoutakaporepoti shuleni.
- (b) **Fomu ya maelezo binafsi ya kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba** wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai. Fomu hii nayo utakabidhi ofisini kwa Mkuu wa shule.
- (c) **Tamko la mzazi /mlezi kukiri kukubaliana na sheria za shule** na kuahidi kushirikiana na shule katika kumuwezesha mwanafunzi kusoma bila vikwazo.

**5.0 Tafadhari soma kwa umakini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI DENDEGO.....!!!!**  
**“BIDII KWA MANDELEO BORA”**

.....  
**FURAHA S. MWASAMBILI**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**  
**SHULE YA SEKONDARI DENDEGO**



SIMU: 0789160787,  
 0622333041,  
 0675468465.

EMAIL:- [sdendego@gmail.com](mailto:sdendego@gmail.com)

Ofisi ya Mkuu wa Shule,  
 S.L.P 23,  
 Kilosa.  
**14 DESEMBA, 2020**

## HATI YA UTII NA SHERIA ZA SHULE.

### SEHEMU "A": (IJAZWE NA MWANAFUNZI)

Mimi .....

Nimesoma nakuelewa kabisa masharti yote na sheria za shule ninazikubali sheria hizo na nitazifuata na kuzitii nikijua kuwa ninaelimishwa na umma kwa manufaa yangu na Taifa kwa ujumla.

Sahihi ya Mwanafunzi ..... Tarehe .....

### SEHEMU "B": (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

Mimi .....

Mzazi /mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu. Ninathibitisha kuwa mwanangu amesoma na kuzielewa sheria za shule. Ninaahidi kuwa nitashirikiiana na uongozi wa shule kuona kuwa mwanangu anafuata taratibu zote za shule kwa manufaa yake na kwa manufaa ya umma.

Pia ninaahidi nitamuhimiza ahudhurie shule pamoja na kusoma kwa bidii maendeleo ya mwanangu.

Anuani ya mzazi/mlezi

.....

.....

.....

Simu: .....


Saini .....

Tarehe .....

**FORM ONE JOINING INSTRUCTION FOR ACCADEMIC YEAR 2021**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**  
**PRESIDENT OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**  
**KILOSA DISTRICT COUNCIL**  
**DENDEGO SECONDARY SCHOOL**

PHONE: 0789160787,  
 0622333041,  
 0675468465.



The Headmistress office,  
 P. O. BOX 23,  
 Kilosa.

EMAIL:- [sdendego@gmail.com](mailto:sdendego@gmail.com)

14 December, 2020

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**FROM:** The Medical Officer  
 Government Hospital

.....  
 .....  
 .....

**RE: MEDICAL CERTIFICATE**  
**(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

I have examined ..... who aspires to join form one in a year 2021 in your school as follows:

S/No.	AREA	REMARKS
01.	Skin	
02.	Eyes	
03.	Ears	
04.	Teeth	
05.	Chest	
06.	Spleen	
07.	Abdomen	
08.	Urine	
09.	Tool	
10.	Hb Haemoglobin	
11.	Sickle Cell	
12.	Asthma	
13.	Pregnancy for Girls	
14.	Any other Comments	

I consider that he/she is physically not physically fit to join your school due to .....

.....  
 .....  
 Signature: ..... Date: ..... Official Stamp: .....

**FORM ONE JOINING INSTRUCTION FOR ACCADEMIC YEAR 2021**